THE HANSARD

Tuesday 26/02/2019

Assembly Building

The Assembly met at 2.30 p.m

The Speaker (Hon. Roba) in the Chair

PRAYERS

NOTICE OF MOTION

HON.ISSACK FAYO (Kinna): County Executive to provide extension services to farmers across the County with emphasis in areas with irrigation scheme for best farming practices such as Rapsu.

HOJA

[MIKAKATI YA UBORESHAJI WA UKUSANYAJI WA MAPATO YA KAUNTI]

MHESHIMIWA YARRROW HASSAN (Burat): Kuwa, ukusanyaji wa mapato ya kaunti ni nguzo kuu ya kuendeleza maendeleo katika kaunti. Kama tunavyofahamu serikali kuu hutupatia fedha kupitia Kwa ukusanyaji wa ushuru, pia hupatia serikali ya kaunti mamlaka ya kusanya mapato na kuyaweka kwa miradi tofauti tofauti ya maendeleo ya Kaunti. Vile tunavyofahamu Kaunti yetu ya isiolo hupata mapato maradufu kwa idara zifuatazo, eneo za kuegeza magari, rasilimali kama vile mchanga, mapato ya ploti, soko ya mifugo na mauzo, na vile vile mbuga za wanyama; ya kuzikitisha ni hali duni ya kukusanya mapato hayo kwa miaka mingi iliyopita. Jumba hili linataka kuimiza idara inayosimamia ukusanyaji wa mapato ya fedha ya Kaunti ya Isiolo, kuweka mikakati imara ili kuboresha ukusanyaji wa mapato kama vile;

(a) Kutekeleza sheria ya kusimamia ukusanyaji wa mapato iliyobuniwa awali,
(b) Kuweka mikakati ya kuzuia wizi wa mapato na wale wanaokataa kutoa malipo,
(c) Kuhakikisha kuna miundo misingi bora na mazingira mazuri ya kufanya biashara,

(d) Pia kukuza na kutangaza mbuga zetu za wanyama kwa watalii wa humu nchini na wa kigeni kupitia vyombo vya habari.
(e) Idara ya Fedha kubuni njia za kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Kaunti pamoja na kuhakikisha kuna wafanyikazi wa kutosha na wenye tajriba kuu ili kuboresha utendakazi.

Mheshimiwa Spika vile unajua sisi mapato yetu kama Kaunti mikakati na uboreshaji was mapato ya Kaunti vile wote munajua ya kuwa Kaunti yetu tulikuwa tukitegemea mbuga ya wanyama ambaye viongozi na watu mashuhuri waliweza kusoma na bursary mpaka mahali tuko.Tumeweza kutangazwa kama baraza *county council* wakati huyo kama namba mbili kwa utajiri kwa sababu ya mbuga ya wanyama na ukusanyanyi wa mapato. Mheshimiwa Spika jambo la kushangaza wakati tumerudi kwa ugatutuzi, ile pesa tuliweka kama ushuru wetu tuliweza kupata nusu. Mheshimiwa spika kwa mfano, pesa tuliyokuwa tukitegememea wakati huo ni ushuru kutoka bunga la wanyama na mchanga.Bwana spika ukienda saa hii hizo barabara ya kwenda kwa mchanga imeharibika, haipititiki, wale wenye magari wanalalamika pamoja na *community* wanaishi uko, juzi kulikuwa na *demonstration* Bwana Spika ambayo watu walisema hawezi kutoa ushuru kwa sababu barabara haipitiki.Kuhusu mambo ya ploti na ardhi, nafikiri tukikusanya ushuru ya ploti peke yake tunaweza hata kupata billioni.Utakuta sehemu kadhaa ikiwemo wodi yangu kama Kilimani, kambi karba ambayo haijafanyika *registration* , wanainchi wanalalamika wakiomba serikali ya kaunti ikuje ifanye *registration* hili wapate cheti ya kuonyesha wanamiliki.Lakini ajabu ni kuwa hiyo mambo tuliacha,hata tulifika mahali ambapo ,mahali ya kulipiti kodi ya ploti haijulikani waliko waliwahama hapo kwa muda tunaweza kusema mwaka, wanainchi hawajui mahali wananenda kulipia ushuru yao, hivi juzi ndio nimesikia kwamba wako kwa *treasury* . Kuhusu wale wanapaswa kuendesha hiyo kazi, kuna hoja ilikuja, kwa saa hizi mtu akikataa kulipa ushuru hatuna uwezo wa kupepelekeka kotini ili kuamuru hiyo pesa ilipwe. Hakuna sheria kwa saa hii tumepitisha kusimimamia ushuru wetu, utakukuta maakaunti zingine, ukikataa kulipa unashikwa na mpaka ulipe ile kodi unatakikana ndiposa unaachaliwa, kwa sasa hatuna uwezo wa kufanya namna hiyo Bwana Spika. Nasikisia kuna msawada ilipaswa kuletwa hapa kwetu kwa lakini haijafikia kwa Nyumba mpaka saa hii. Mambo ya soko saa hii nikuwa tegemeo kubwa ni mifugo, tunajua kuna soko lakini mahali mingi haijafilkia, juzi nilikuwa mkutano ya usalama huko Ngarentare na kuna soko ambayo wananchi wamejifungulia kwa hiari yao, niliuza kama kuna mtu wa

serikali ya kaunti anaokota kodi, lakini niliona ni wanainchi wenyewe ndio wanafanya kazi hiyo ,wanainchi walisema hakuna afisa yeyote ameifika uko, hiyo yote ni changamoto ambayo tunahitaji kuboresha.Kwa hayo naomba mheshimiwa Ekuwam aweze kuniunga mkono, ili tuonge juu ya jambo ambayo ni muhimu sana asante.

MHESHIMIWA EKUAM TERU (Ngaremara)**:** Asante sana Mheshimiwa spika, mimi naunga hii hoja mkono, hii mambo vile mheshimiwa amesema ni kweli. Hatuna sheria ambayo inasaidia watu wote kufuatilia hasa mapato amabayo kaunti yetu ingeweza kupata. Kwa mfano hii mambo ya kuegeza magari, mambo ya ploti. Kujiandikisha kama maploti zote za hizi wodi zote, hata hii sehemu ya Ngaramara, *town* hapa, kuna hii mambo ya *registration* ambayo kaunti ingepata pesa, lakini haijawezekana na huko wananchi wanaongoja na kutamani lakini mwenya kufikiya huko hajapatikana. Kwa mfano kama soko ya mifugo ambayo tunauza mifugo yetu hata hapo kuna shida ambayo inatakikana irekebishwe. Pia kuna hii mambo ya mchanga, shangarawe ambayo inaokootwa kwa sehemu yetu, na hiyo pia hakuna sheria inafuatiliwa, hiyo mchanga ni kama watu wanapora na *community* yetu hawafaidiki. Kwa hivyo Bwana Spika hii ingewezekana tuu kama kuna mswada iweze kufufuliwa hili tuweze kuchunga rasmali yetu. Kwa sababu kuna pesa inatoka kwa sehemu hizo lakini hakuna mtu anafuatilia kwa sheria. Mimi sitasema mengi sana, kwa sababu

Waheshimiwa wanakula *mori* kwani hi hoja ni muhimu na ni ya faida hasa kwa hii kaunti yetu, bwana spika naona nitakomea hapo, na nashukuru mheshimiwa mabayo amelete hiyo hoja katika hii nyumba, asante.

(Question proposed)

MHESHIMIWA IDD HASSAN (BULAPESA): Asante Bwana Spika, nasimama kuunga mkono hoja hii ya ukusanyaji wapato ya kaunti ambayo imeletwa na mheshimiwa Yarrow.Nadhani hivi majuzi sisi wote tulishuhudia kuwa kaunti ya Isiolo ndiyo namabari ya mwisho kwa ukusanyaji wa kodi.zile pesa zinapelekwa huko ni kini 0.2% na njia mingi ambayo tunaweza kuhimariarisha mapato yetu, isipokuwa tu inataka kujitolea katika serikali yetu ya *Executive* hili iweke mikakati.Tukiangalia hapo awali tulikuwa nambari ya kwanza katika ukusanyaji wa ushuru. Ukiangalia vizuri ilikuwa imechangiwa na mbuga zetu za wanyama ambazo baadaye wale wageni waliokuwa wanakuja

walisita kwa sababu ya hali ya usalama. Lakini sasa tukiangalia kuwa kuna nafuu katika hali ya usalama, jinsi walivyo kuwa wana vamiwa kwa barabara ,kwa sasa ni jukumu ya serikali kufamisha wageni kwamba hali ya usalama ni shwari hili tupate wageni.Katika *town* yetu kuna njia mingi ukiangalia katika Kaunti zingine huwezi kupita bure, kama unafanya biashara mpaka utoe ushuru.Lakini wale wanatoka kwa kaunti zingine wakiwa wanafanya biashara, wanauza na kupata faida marudufu na kuondoka na yote.Kwa sababu wale wamepewa jukumu hii wamezebea. Naunga hoja hii mkono na hata kama itabidi waweze kuweka mvumo wa *digitali* hili kuona ya kuwa hile pesa inapotea katikati haipotei, hivyo basi kupunguza hasara na tunaweza kupata mapato zaidi, nashukuru bwana spika.

MHESHIMIWA ISSACK FAYO (Kinna)**:** Ahsante Mheshimiwa Spika, hata mimi nitajaribu kuongea Kiswahili. Hii mambo inaongelewa hapa ni muhimu sana, ya kwanza inatukumbusha yaliyopita, tena inatupea tahadhari vile tuko saa hii. Bwana spika samani bwana spika mimi na pengine wote wako hapa kwa hii nyumba na hata mimi wamefaidika na msaaada ya kaunti ya *bursary*.Hiyo pesa ilitoka kwa ushuru uliosanywa *na county council* hile ya samani.Bwana spika mahajabu ni kuwa wakati ugatuzi umekuja na pesa imekuwa mingi,macho ya watu wote imerudi kwa ile pesa serikali kuu inatupatia na tukaacha kusanya ushuru yetu ya ndani.Hiyo ni hatari kubwa sana kwa maendeleo na mpangilio ya siku ya mbele ya Kaunti yetu.Tunahitajika tuwe na sheria ya kuzuia na kukaza namna ya kupata mapato, kwa mfano sheria yetu ya kuokota ushuru saa hii haina vipengele ya kupeleka mtu kotini kama hatakosa kulipa.Hali hiyo aipei motisha wakusanyaji ushuru kwa sababu wakikushika na hakuna mahali watakupeleka hivyo basi haitawafanya wengine walipe ushuru.Hii sababu inafanya mahali magari yanaegezwa hakuna pesa inaokotwa, watu wana kuja na mahali yao wanauza na kuondoka na hakuna ushuru wanalazimishwa kulipa, hayo yote yanatokana na kukosa sheria. Sheria ambaye inaadhibu wenye wameshindwa kulipa ushuru, ukiona manyumba zetu ambazo imejengwa *Isiolo town*, na Isiolo kaunti yote hatulipi ushuru, hiyo pesa vile mheshimiwa aliolete hoja hii, inaweza kuwa mabillioni kila mwaka ikizingatiwa.Hapa Isiolo kuna njia nyingi wangeweza kujua watu wangapi hawajilipa ushuru wa manyumba, kwa sababu manyumba yote ya Isiolo iko kwa mpangilio ya maji, kuna chache wako kwa mpangilio ya maboba ya maji taka. Bwana spika kama hiyo rekodi ingefuatwa na kuhakikisha wale wote wameunganishwa na maji, na hiyo yote ni aridhi ambayo imekuwa *registered*

Bwana spika watu wetu wanafaa kufunzwa, ukienda Kaunti tunapakana nao, utakuta katika mita yao utapata wakusanyaji ushuru wako kwa kila mahali, na hawa watu wakusanyaji wa ushuru wako na bidii sana, na vile sio ile ya kupeana pesa taslimu ni tarakilishi kaunti inapata hiyo pesa asimilia mia kwa mia.Bwana spika sioni kama kuna hasara kuandikisha na kuajiri wafanyi kazi wengi kwa hiyo idara ya ukusanyaji wa ushuru. Bora wapewe kadiri ya pesa inayotakikana kwa siku, na ikaguliwe na wale watashindwa kufikisha hiyo kiwango wamepewa waadhibiwe.Bwana spika mengine itakayozaidia hii kaunti kupata pesa , ni usaidizi wa marafiki na kama jana tulikuwa kwa mkusanyanyiko ambayo benki ya dunia ilikuwa ikikagua miradi zake.Kulingana na utaratibu niliona pale hii kaunti iliweza kupata takrban shillingi million mia nne kwa sekta tofauti, tofauti.Bwana wafadhili wanaweza kusaidia, amabo tukiwa tafuta watatusaidia kutimiza mahitaji ya kaunti yetu, kwa kufanya hivyo pesa ambazo imetengewa kwa kufanya kazi itakayo fanywa na wafadhili itaenda kwa kazi ingine.Bwana Spika njia nyingine ni kuhakikisha kuwa ushuru sio juu sana.Ukienda kwa masoko kadhaa za dunia, ukindea kwa viwanja vya ndenge bei ya vitu iko chini,watu wengi wanunua vitu kwa uwanja wa ndenge kwa sababu bei ni chini, kwa sababu ziko ghali kwa maduka. Bwana Spika ushuru yetu ikipungua italete bei ya bidhaa kwenda chini na itafanya motisha kwa wafanyibiashara na kutokana na hiyo tutapata ushuru ya juu kwa siku. Bwana spika nataka kuongelea juu ya Bisanadi, umuhimu wa bisanadi kwa hii kaunti kwa miaka saba na kwenda juu ni kuangamiza watu wa Kinna.Watu wa Kinna wamesanyana kwa polisi na kusalitiiwa na kufungwa juu ya Bisanadi haifanyi biashara ya utalii. Bisanadi haisaidiwi nah ii kaunti, hakuna askari wa kaunti hata mmoja hako Bisanadi, Bisanadi imetupwa, iko pale kwa kuangamiza watu wa kinna.Bisanadi kama hawezi kurudishwa na iweze kufanya kazi inayotarajiwa ,hiyo ardhi imepokonywa watu wa Kinna, ingekuwa muhimu hata warudishwe.Sisi watu wa Kinna tumejitolea, tumepea wanyama wa pori maji, tumepea makao,nyasi ,bwana spika wakati nyasi yetu inaisha na sisi tunaenda Bisanadi, Bisanadi ambayo hakuna kitu inasaidia kazi na haina faida kwa kaunti ya Isiolo,watu yangu wanashikwa na hiyo ushuru awaleti Isiolo hiyo inafaa kuangaliwa .Kamati uhusika na ,mambo utalii itusaidie itatue hiyo maneno.Sisi kama kaunti tulilete mikakati mingi sana kama *RRI (Rapid Response Initiative)* iliweza kukaguwa sekta tofauti,tofauti baada ya siku mia moja.Tuliamua mambo wa kadha wa kadha ya umuhumi ambayo tulitambua kabla, tuikague baada ya siku mia moja.Bwana spika hiyo tunajua hata *members* wanajua

ilifanyika.Bwana spika upande wa serikali wangeanzisha tena kitu kama hiyo ambayo inapea motisha kwa wafanyi kazi hasa kwa wakubwa wa sekta tofauti, tofauti waambiwe kile wanapaswa kufanya na kutumiza kwa muda fulani.Bwana spika watu wasipofanyiwa hivyo wata kuwa wana lala kazini .Bwana spika kuna methali yetu ya kiborana *(vernacular*) kama hatutafanya hayo yote itakuwa kitu kama hiyo asante sana.

MHESHIMIWA DAVID LEMANTILE (Oldonyiro)**:** Asante sana Bwana Spika, nasimama kuunga hoja hii mkono, ni muhimu sana kwa kwa Kaunti. Kulingana na mpangalio wa serikali ya kaunti, mpangilio yao ya kuokota pesa ni kama haiko. Ukiona kwa runinga Kaunti nyingi wanaonya na wanaambia watu wao walipe ushuru, la sipo wataadhibiwa, lakini Isiolo hawajafanya hivyo. Jambo hili haijawekwa maanani. Bwana Spika vile najua tuko na sheria ambayo tumeweka ambayo inaisaidia Kaunti kuokota kodi, lakini vile mheshimiwa Yarrow amesema hiyo sheria haijafanya kazi, ndio maana sisi wote tunaangalia serikali kuu lakini hatuangalii kile tunaokota .Hii ni Kaunti tajiri sana tuko na mbuga za wanyama, mahoteli na mifugo yetu yote.Ukienda soko ya kuuza matunda . nguo kukuu,ukiona watu wanauza hizo nguo wengi wao sio wa Isiolo,tukikubali wakuje wauze tunasema ni soko uhuru hakuna kuokota kodi .Bwana spika watu wetu hawatajua umuhimu wa kufanya hiyo kazi.Ni jukumu la serikali kuchunga watu wake, Jukumu la serikali kuhakikisha wale wanafanya biashara ndongo ni watu wake .Mheshimiwa spika hata saa hii tukienda kuuza ngombe ,Tigania ukitoe ngombe ukipitia hapo unalipia kodi hata kabla ujafika soko , na ilo haifanyiki hapa Isiolo.Utakuta ngombe imetoka kaunti ya Samburu na inauzwa hapa *free* sisi tunaokota shilling hamsini, lakini wewe jaribu peleka ngombe sokoni kuuza , wewe kama sio mwenyeji unalipa shillingi mia moja, wale wanalipa shillingi ishirini au hamsinii .Hii ni muhimu kama tunaweza shikilia hoja hii imeletwa na mheshimiwa Yarrow .Sisi tuko na mpangilio kama bunge la Kaunti , umeona tukikuja na hoja hii tunataka watu wetu waimarike na Kaunti ipate pesa, lakini serikali ya kaunti ikiongozwa na gavana wanalalai masikio.Kazi yao ni kuangalia kile itatoka kwa serikali kuu, hii ingine hawajui.Sasa kama hatuwezi kujitaidi tunaongoja tu tupewe mheshimiwa spika hiyo haitakuwa kitu mzuri, tutabaki tukilia , tukikorogana ,tukisema hii na hii lakini kaunti zingine zinaendelea mbele kwa sababu wanaokota kodi yao kulingana na mpangilio yao. Mheshiwa Spika walisema wanaokota kodi kwa kutumia mvumo wa tarakishili, enda kwa maduka, au soko la ngombe, risiti inayoitwa imeandikwa baraza la Isiolo bado inatumika, mimi naweza

kudhibitisha hayo kwani niliandikiwa mimi mwenyewe. Nilienda kununua ng'ombe nikapewa hiyo risiti imeandikwa baraza la Isiolo, hiyo ni kuonyesha hakuna kitu inafanyika hapa. Hayo ,*machine* ya *digitali i*linunuliwa kwa pesa zaidi million arubaini,haifanyi kazi kwa sasa.Mhesheshimwa spika tunasema kama ujipendi na hatakupenda sisi tutapiga kelele tuhimiza serikali ifanya hivi na hivi mwishowe wao ndio watatekeleza vile tunasema, hii haisadi mimi kama mheshimiwa Lemantile au wewe, mbali inasaidia serikali yetu na watu wetu. Mheshiwa Spika ukiangalia barabara ukitoka Nanyuki saa hii haipitiki kwa sababu ya msogomano ya watu, lakini asmilia tisini sio watu wa Isiolo,ikifika saa kumi na moja ,kumi na mbili wanafunga mizigo kwa magari yao na kuondoka, asubuhi mapema wanakuja na magari.Mheshimiwa spika ni muhimu serikali ichukuwe jukumu ili na kuhakikisha ya kwamba kodi inapiwa kulingana na mpangilio ya serikali , wenyeji wamepewa nafasi ya kufanya biashara yao hiyo ndio itainua watu wetu, watu wengi wanakuja tunajua ni wanununzi wa mbonga hatuko kwa ukulima.Mheshimiwa Spika naunga hii hoja mkono na naomba kama ikiwezekan serikali itekeleze hoja hii nashukuru.

HON. MOHAMED JIRMO (Cherab)**:** Thank you Mr. Speaker, *(inaudible*) … livestocks markets and sand harvesting. I think was during the defunct County council that taskforce was put in place to target tax collectors, the target should be given on how they normally collect revenue during the day.Sand harvesting was going on during the night, the revenues clerks were given security so that the revenue does not get lost during the night.The introduction of automated machines should be put in place to seal all loopholes so that no money get lost.Our revenue policy should be put in place for the revenue to be improved increased from the game reserves . I was one of the revenue clerk in the game reserve, but the following reduced revenue collection from game reserve; charcoal burning within the game game reserve, cattle grazing, cattle rustling, poaching, lack of marketing of the game reserve and lastly lack of motivation of staff, also rangers should be employed because those who are currently working are 45 years and above. If all this things will be tackled the visitors will come and the revenue will improve, employment of revenue clerks if needed should be done within the game reserve, so that we get enough revenue

MHESHIMIWA YARROW HASSAN (Burat)**:** Asante Bwana Spika, nashukuru Waheshimiwa wenzangu kuunga mkono hoja, nilikuwa wakati wa baraza la Isiolo *(county council)* kuna taskforce ambayo tuliunda , kwa mfano tu

mambo ya mchanga tulipata ta kuwa lori ambayo inakuja kuchukua muchanga ni kama lori mia moja na ishirini, ni wakati ile hakuna kazi, hiyo magari mia moja ishirini ikipiga *trip* moja ni shilling elfu moja na ishirini kwa siku,ambayo ni ni million tatu elfu misa kwa miezi , million aroubaini tatu , elfu mia mia saba kwa mwaka. Ni hiyo tu tulihesabu mchana, Je tungepata hii mapato, wakati huo tungeweza kuokota hata shilling million mia tano kwa mwaka , lakini mambo yametushangaza ni kuwa hatumwezi kupata hata shilingi milioni mia moja .Nafikiri tu Bwana Spika kama kichinjio , nafikiri members wale walienda mulienda enda, inakaa kwa mazingara ya kutatanisha sana, sisi c*ommunity* tunachi huko ile matatizo ni mingi sana , na mimi nikiwa kiongozi , hata wakati ni nili kuwa *councillor* nilipendekeza hiyo kichinjio ibinafisishwe , hii ile tunapata saa hii mfanyi bishara wa kinanafsi anaweza kulipa hiyo pesa utakuta community wanapata mapatapo kubwa kuliko sasa. Nafikiri Bwana Spika nitaweza kulete hoja wakati nyingine hili hiyo kijichichinjio iweze kubinafsishwa. Na vile members wamechgangia kuhusu wachuuzi wengi kutoka mahali nyingine wanafanya biashara bila kutoa kodi yoyote ni mambo ya kushangaza. Bwana spika hii *town* yetu ambayo ni munisipaliti haipati ushuru kwa sababu watu wanauza kando kando ya barabara .Hebu Bwana Spika angalie hii kampuni ndogo ya maji *IWASCO* wanapata pesa nyingi na hiyo tu ni pesa ya maji, utakuta hiyo kampuni imendelea kimaisha, wafanyi kazi wanalipwa kwa wakati, na wameimarika kiuchumi ni pesa ya maji pekee.Je kama utajiri wote tuko nao tungeokokota pesa , wanainchi wangepata huduma na kaunti ingeimarika kiuchumi, kwa hayo nashukuru wenzangu waliounga hii hoja mkono, naomba iweze itekelezwe asanteni.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

HON. SPEAKER: The house stand adjourned until tomorrow 9:30 a.m.

The House rose at 3.55 p.m